TANGAZO LA SERIKALI Na. 999 La Tarehe 6/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA NDONGOSI KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA WA NDONGOSI YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo Msitu wa Ndongosi kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndongosi ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

**2.** Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndongosi.

Madhumuni ya tangazo

**3**. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza eneo la Msitu wa Ndongosi kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu ya uwanda wa juu, nyasi, miti ya miombo, vyanzo vya maji na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baianuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

**4**.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au

mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndongosi.

Uwasilishaji wa pingamizi

**5**. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kuanzisha Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndongosi, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

JEDWALI


*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA SONGEA

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA NDONGOSI

Makadirio ya eneo: Hekta 1186.58 au Kilometa za Mraba 11.87

Unakopatikana na Mipaka:
Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Ndongosi unaopatikana Wilaya ya Songea katika Mkoa wa Ruvuma kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 3141 (Skeli 1:20,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*